

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU



Unapojibu tafadhali taja:

10/11/2023

**TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE WA HALMASHAURI YA
WILAYA YA BAHU**

Mkurugenzi Mtendaji anawatangazia watumishi wote kuwa, kutakuwa na zoezi la kusahihisha taarifa a Kiutumishi na Mishahara (Data Cleaning) kwa watumishi wa Umma kuanzia tarehe ya tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 16/11/2023.

Hivyo watumishi wote wenye tarehe za kuzaliwa zilizokosewa wanatakiwa kuwasilisha taarifa sahihi ili zibadilishwe, taarifa hizi ziambatishwe nav yeti vya kuzaliwa, na kitambulisho cha Taifa.

Aidha, watumishi ambao hawakuwasilisha namba zao zao za simu, email zimekosewa au hawana kabisa, ambao hawakuwekewa masomo wanayofundisha katika mfumo wa HCMIS wanatakiwa kuziwasilisha kwa ajili ya kuzifanyia kazi katika mfumo shirikishi wa usimamizi wa rasilimali watu na usimamizi wa mishahara HCMIS.

Kwa Mujibu wa maelekezo ya Katibu Mkuu Utumishi baada ya zoezi hili kukamilika hakutakuwa na nafasi nyingine ya kurekebisha taarifa za kiutumishi kwa wale ambao hawatawasilisha taarifa zao.

Taarifa hizi mziwasilishe kwa Wakuu wenu wa Idara kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 13/11/2023.

Zaina M. Mlawa

MKURUGENZI MTENDAJI (W)